

OFISI YA RAISI TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
(TAMISEMI)

SHULE YA SEKONDARI MNARA
S. L. P 445,
LINDI.
MOB: 0655386568/0686070896

BARUA PEPE: kessanta@gmail.com
10/12/2021

MZAZI/MLEZI WA _____
S. L. P 328
LINDI.

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MNARA MWAKA
2021**

1. UTANGULIZI:

Ninafurahi kukuarifu kwamba mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2021 katika shule ya sekondari Mnara Hongera sana.

Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tar 11/01/2021. Mwanao anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 11/01/2021. Huapaswi kumchelewesha hata siku moja kwani ufundishaji utanza tarehe 11/01/2020 ambayo ndio siku ya kufungua shule.

Ili kuepusha usumbufu hakikisha unamwandalia mwanao mahitaji yote yaliyoainishwa na kumwelekeza azingatie maelekezo yote katika barua hii.

2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

A. SARE ZA SHULE

- I. Sare ya shule hii ni **SHATI 2 NYEUPE, SURUALI 2 ZA KAKI NA VIATUVYEUSI** pamoja na mkanda mweusi wa ngozi laini kwa wavulana na **SHATI 2 NYEUPE, SKETI 2 ZA KIJANI NA VIATU VYEUSI** kwa wasichana. Pia tuna ruhusu **HIJABU NYEUPE** iliyoshonwa kiufasaha.
Mishono ya sare zote **ZISIWE ZA KUBANA**.
- II. Sare ya michezo kwa **KIDATO CHA I 2020** ni **TSHIRT NA BUKTA BLUE** wavulanana **TSHIRT NA TRACK BLUE** wasichana.
Raba na soksi za michezo rangi yoyote.

B. VIFAA KUJIFUNZIA

Madaftari (counterbooks) kumi (10), tisa quire 2 na moja quire 4. Qure 4 ni maalumu kwa ajili ya jaribio la wiki linalofanyika kila ijumaa.

mkebe, peni za kutosha na file la plastiki

Begi la kuwekea daftari.

Dictionary: English to English dictionary.

N.B: MWANAFUNZI ATAONESHA VIFAA VYOTE VYA KUJIFUNZIA NDIPO APOKELEWA

C. SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Shule inazingatia miongozo inayotolewa na wizara ya Elimu.

Hivyo zingatia mambo ya msingi ya fuatayo:

- i. Kila mwanafunzi anawajibika kuwa na heshima na adabu kuanzia nyumbani, shuleni na mtaani.
- ii. Mwanafunzi haruhusiwi kutumia lugha mbaya, matusi, kati yake na mwanafunzi mwenzake kwa mwalimu na wengineo.
- iii. Ni lazima kuonesha moyo wa kushirikiana, huruma, upole na kusaidiana katika shughuli mbalimbali pamoja na kazi.
- iv. Mwanafunzi anatakiwa kusimama na kusalimia na kupokea mzigo wa Mwalimu au mtu yeyote anamzidi umri.

D. WANAFUNZI HAWARUHUSIWI KUFANYA MAMBO YAFUATAYO:

- i. Kuvuta sigara au bangi
- ii. Kuvaa mavazi yasiyo ya heshima
- iii. Kutumia madawa ya kulevya
- iv. Kupiga kelele darasani na nje ya darasa
- v. Kufuga kucha ndefu, kuwa nanywele zisizokubalika na chafu, kuvaa mapambo, kujipamba rangi katika kucha na midomo (wasichana)
- vi. Kunyoa nywele katika mitindo isiyokubalika
- vii. Kuchelewa kufika shuleni nakufanya usafi katika eneo alilopangiwa
- viii. Kuchomekea na kuvaa mkanda ni azima
- ix. Ni marufuku kuvaa viatu vya wazi (SANDALS)

E. MAKOSA YAYOWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE KWA MWANAFUNZI

- i. Wizi
- ii. Uasherati, ubakaji na ushoga
- iii. Ulevi
- iv. Kudharau bendera ya Taifa
- v. Makosa ya jinai
- vi. Kupiga au kupigana

- vii. Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma
- viii. Kuoza au kuolewa
- ix. Kupata au kusababisha Mimba ndani au nje ya shule
- x. Kutoa Mimba
- xi. Kugoma, kuchochea, kuongoza na kuvuruga amani na usalama wa watu
- xii. Kukataa adhabu kwa makusudi
- xiii. Matumizi mabaya ya Lugha kwa walimu na watu wengine

F. **UNATAKIWA KUKAMILISHA/KUJAZA MEDICAL EXAMINATION FORM** ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali. Fomu hiyo ikabidhiwe kwa Mkuu wa shule mara utakapowasili shuleni.


G. **MAMBO YA KUZINGATIA SIKU YA KURIPOTI:**

1. Fika na cheti cha kuzaliwa.
2. Fika ukiwa umevalia sare ya shule.
3. Fika na joining instructions uliyopewa kabla ya kujiunga na shule.
4. Fika na mzazi wako au mlezi anayekugharimia mahitaji ya shule.
5. Fika na namba za simu za mzazi wako au mlezi
6. Hakikisha unapokelewa ofisini kwa mkuu wa shule

H. Tafadhali soma

kwamakinimaelezo/maagizohayanakuyatekelezakikamilifu

KARIBU SANA MNARA SEKONDARI



STEPHEN KESSANTA PIUS

MKUU WA SHULE

MNARA SEKONDARI

**MKUU WA SHULE
MNARA SEKONDARI
LINDI**

STUDENT MEDICAL EXAMINATION FORM

MEDICAL OFFICER

HOSPITAL

NAME OF STUDENT

AGE

Please examine the pupil and give us report regarding his/her suitability for secondary school studies.

1. Blood
2. Stool
3. T. B Test
4. Syphilis test
5. Urine examination
6. Eye test
7. Chest
8. Ears
9. Spleen
10. Abdomen
11. Pregnancy (GIRLS ONLY)

I have examined and consider that he/she is physically and mentally fit/unfit for further studies.

Name: _____

Signature

official stamp

date